Jarida La MELI

TOLEO LA 5 JULAI - SEPTEMBA 2022



MSCL YAKABIDHIWA MELI MPYA..

UK. 2



ALIYONENA KINANA BAADA YA KUTEMBELEA MIRADI..

UK. 4



MV LIEMBA YATENGEWA BIL 8.1 KWA AJILI YA UKARABATI...

UK. 9



MWENYEKITI WA BODI ATAKA UFANISI BAADA YA KUPOKEA MELI

Na. Abdulrahman Salim

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Meja Jenerali Mst. John Mbungo amewataka watumishi wa Kampuni hiyo kufanya kazi kwa ufanisi ili kuongeza pato la Kampuni pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

Amesema kuwa Serikali imeonesha nia ya kuipa uwezo Kampuni hiyo kwa kuwakabidhi meli tatu zilizokuwa chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA) ili kuweza kuziendesha, hiyo ikiwa ni ukamilifu wa hatua mojawapo kati ya makubaliano kadhaa ikiwemo kukabidhi baadhi ya miundombinu inayoendana na utendaji kazi wa meli hizo.

"Wafanyakazi wa MSCL kwakweli niwatake sasa wabadilike, kwa sababu Serikali inaonesha uwezo wake wa kuweza kufanya mabadiliko ndani ya Kampuni, kwahiyo sisi hatuwezi kubaki tena nyuma, lazima tubadilike, tufanye kazi kwa bidii, kwa maarifa na juhudi ili tuweze kuzalisha," Alisema.

Hata hivyo, Meja Jenerali Mbungo alisisitiza kuwa watumishi wa MSCL hawana sababu ya kusuasua katika utendaji kazi na hivyo kuwaasa kutorudi nyuma na kuzisimamia vizuri meli hizo walizokabidhiwa.

Inaendelea Ukurasa wa 8..



MSCL YAKABIDHIWA MELI NA TPA

Na. Abdulrahman Salim

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA) imeikabidhi Kampuni ya Huduma za Meli nchini (MSCL) meli tatu zinazotoa huduma katika Ziwa Nyasa ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa lengo la kuziweka meli hizo katika usimamizi madhubuti wa MSCL.

Meli hizo za MV. Njombe, MV. Ruvuma pamoja na MV. Mbeya II zilizogharimu Shilingi Bilioni 20.1 zimekuwa zikisuasua katika kutoa huduma kwa wananchi wa mwambao wa Ziwa Nyasa pamoja na nchi jirani kutokana na TPA kujikita zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya usimamizi wa bandari nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi sekta ya Uchukuzi Bi. Stella Katondo alisema kuwa TPA imekuwa ikisimamia meli hizo ili kuhakikisha wananchi wanaozunguka Ziwa Nyasa wanapata huduma ya usafiri kutoka eneo moja kwenda eneo lingine lakini usimamizi wa meli ni jukumu la msingi la MSCL.

"MSCL imeanzishwa na Serikali kwa ajili ya usimamizi wa meli zinazomilikiwa na serikali nchini. Aidha, kwa kipindi kirefu sasa MSCL imekuwa ikisimamia meli za Serikali na kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Hivyo ni matarajio ya Serikali kwamba baada ya meli hizi kukabidhiwa kwa MSCL zitasimamiwa ipasavyo na kutoa huduma iliyokusudiwa," Alisema.

Wakati akitoa taarifa ya meli hizo Mkurugenzi Mkuu wa TPA Bw. Plasduce Mbossa alisema kuwa meli za mizigo za MV. Njombe pamoja na MV. Ruvuma zilianza kujengwa mwaka 2015 na kumalizika mwaka 2017 na kugharimu Shilingi Bilioni 5.5 kila moja huku zikiwa na uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja.

"Kwa upande wa meli ya MV Mbeya II ambayo ni meli ya abiria na mizigo, Mamlaka ya Usimamizia wa Bandari ilianza ujenzi wa meli hii mwaka 2017 kwa gharama ya shilingi bilioni 9.1 na ujenzi huo ulikamilika mwezi Oktoba,2020. Meli hii ilijengwa na Mkandarasi Songoro Marine na baada ya kukamilika ilianza kutoa huduma katika bandari za Ziwa Nyasa kupitia vituo 13 kuanzia bandari ya Kiwira hadi Mbamba bay na kurudi," Alisema.

Akitoa neno la shukurani kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL Nahodha Bembele Ng'wita aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kuhamisha umiliki wa meli hizo kutoka kwa mamlaka iliyojenga kwenda kwa taasisi yenye uzoefu wa kuendesha meli hizo.

"Kama MSCL tunasema as ante kwa hilo na kusaini hati ya makabidhiano ni ishara ya wazi kwamba sisi tumepokea kwa shukurani na tunaiahidi Serikali kwamba tutatekeleza majukumu yetu ya msingi, lakini pia tuwaahidi wananchi wanaotegemea huduma ya usafiri katika mwambao wa ziwa kuwa watapata huduma safi, salama, bora na kutoa ufanisi katika shughuli za usafirishaji," Alisisitiza.

Akipaza sauti za wananchi katika hafla hiyo fupi ya makabidhiano, Mbunge wa Jimbo la Kyela Mhe. Ally Mlaghila alisema kuwa wananchi hawajali taasisi inayosimamia meli hizo isipokuwa wanahitaji kupata huduma nzuri nay a uhakika.

"Tunachotegemea sasa ni kwamba MSCL mnaenda kututoa hapa tulipo kutupeleka hatua nyingine mbele, tumieni masoko yaliyopo, tunaomba msiache soko la Malawi, endelezeni walipoishia TPA katika kuhakikisha meli hizi zinafanya kazi."

Tukio hilo la makabidhiano limefanyika tarehe 06.09.2022 baada ya pande zote mbili kutia saini hati ya makabidhiano ya meli hizo, tukio ambalo limeshuhudiwa na vyombo vya serikali ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Ofisi ya Mwanansheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya pamoja na Mbunge wa Jimbo la Kyela, na Diwani wa Kata ya Kajojomole katika bandari ya Kiwira.

NAIBU WAZIRI MWAKIBETE ATOA MAAGIZO KWA BODI YA MSCL

Na. Abdulrahman Salim

Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete ameiagiza bodi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuhakikisha wataalamu wa ufundi wa Kampuni hiyo wanashiriki kufanya ukaguzi wa mitambo wakati ikiwa kiwandani inakotengenezwa ili kuepusha changamoto ya kuletewa vifaa vilivyokwishatumika na kuipa serikali hasara.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ukarabati wa meli ya MT. Sangara mkoani Kigoma Mhe. Mwakibete alibaini uwepo wa baaadhi ya vifaa vilivyokwishatumika na kusisitiza kuwa Serikali haitaipokea meli hiyo itakapokabidhiwa endapo itagundulika kuwa na mapungufu na hivyo kutoa mwezi mmoja kuhakikisha vifaa hivyo vinaondolewa na kuwekwa vifaa vipya.

"Tunataka ndani ya mwezi huu, viwe vimeshashushwa, sijajua atatumia muda gani 'ku-order' lakini ndani ya mwezi wa 9 mpandishe tena hapa, tukija mwezi wa 10 na kuna ziara za viongozi wakubwa katika mkoa wa Kigoma wakija hapa tunategemea tayari spea ziwepo mpya sio tena hizi used (zilizotumika) , sijui tunaelewana vizuri?" Alisisitiza.

Naibu Waziri Mwakibete amesisitiza umuhimu wa watalam kukagua kwa karibu ukarabati huo mkubwa unaofanyika ili kuhakikisha maboresho yote yanayofanyika yanafanywa kwa kufuata vipengele vya mkataba.

Akizungumzia vifaa vinavyotiliwa mashaka Mrakibu wa Meli za MSCL Mhandisi Abel Gwanafyo alisema kuwa kuna vifaa kadhaa ambavyo vinaonekana kuwa vimetumika na mkandarasi tayari ameshaviweka kwenye meli kwaajili ya kutumika.

"Kuna jenereta ya dharura, ipo imepandishwa lakini tunaona kwamba imetumika, tuliikagua, tuliona baadhi ya pump zinaonekana zimetumika, zimekuja injini mbili za kuendesha meli, hizo ni mpya lakini zinakasoro ya kwamba zinazunguka upande mmoja na 'Gear box' zake zinazunguka upande mmoja, hiyo tukaona tumsubiri yeye atupe namna atakavyoweza kuziunganisha ili tupate tunachokitaka," Alieleza.

Meli ya MT. Sangara imefikia asilimia 66 huku Mkandarasi KTMI Co.Ltd ya Korea Kusini akiwa amelipwa asilimia 15 ya gharama za mradi huo ambazo ni sawa na shilingi bilioni 1.2 wakati mradi huo ukigharimu shilingi bilioni 8.4 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2022.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) Mhe. Atupele Mwakibete (wa pili toka kushoto) akitoa maelekezo kwa Bodi ya Wakurugenzi wa MSCL mbele ya Mwenyekiti wa Bodi hiyo Meja Jenerali Mst. John Mbungo pamoja na menejimenti ya MSCL alipotembelea mradi wa ukarabati wa meli ya MT Sangara, Mkoani Kigoma.

Aliyonena Kinana Baada Ya Kutembelea Miradi Ya Mv Mwanza Na Mt Sangara

Na.Mwandishi wetu

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, amesema ujenzi wa Meli ya MV Mwanza unakwenda vizuri na anatamani kuwa miongoni mwa watu wa kwanza watakaiopanda baada ya ujenzi wake kukamilika.

Akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 jijini mwanza Septemba 5, 2022, Kanali Kinana pmoja na mambo mengine alitembelea mradi wa ujenzi wa meli hiyo na kuridhika na hatua kubwa iliyofikiwa na mradi huo.

"Hongereni ndugu wafanyakazi kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya ya kuijenga meli hii na ikikamilika mimi nitakuwa wa kwanza kuja kupanda," amesema akiwa katika eneo hilo ambapo ujenzi wa meli hiyo ambao umefika asilimia 70.

Awali akielezea maendeleo ya ujenzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MCSL) Erick Hamissi, amesema kuwa uunganishwaji wa meli hiyo umefanywa na watanzania 200 walioajiriwa kutekeleza mradi huo

"Ujenzi wa meli hii ulitakiwa ukamilike ndani ya miaka miwili lakini chelezo ndio ilichelewa Kukamilika kwani ilikuwa chelezo ianze lakini vilienda pamoja, mradi huu wote unafanyika hapa hapa kwa hiyo tumepata teknolojia mpya. Sasa hivi hatua tuliyofikia ya hii meli ni kuizindua, kuiweka majini, kuipaka rangi na mwisho wa mwezi wa 11 itaingia kwenye maji, hii ni hatua kubwa sana kwa ujenzi wa meli.

Meli ya MV Mwanza itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo na magari 3 makubwa na magari madogo 20. Meli ina urefu wa mita 92.6, upana wa mita 17, na kina cha mita 20.

Pia itakuwa na madaraja sita ambapo daraja la kwanza litakuwa na watu 60, Daraja la Biashara watu 100, Daraja la Pili watu 200, Daraja la Uchumi watu 834 huku daraja la hadhi ya juu (VIP) watu wanne na vyumba viwili kwaajili ya watu mashuhuri na hivyo kufanya jumla ya watu 1,200.

Pamoja na Kutembelea mradi wa meli ya MV Mwanza, mapema tarehe 2 Septemba, 2022 Ndg. Kinana pia alitembelea mradi wa ukarabati wa meli ya Mafuta ya MT Sangara iliyopo Ziwa Tanganyika, Mkoani Kigoma na kufurahishwa na maendeleo ya mradi huo uliofikia asilimia 66 ya utekelezaji na kuishauri MSCL kukopa ili Kampuni iweze kujiendesha kibiashara.

"Sikilizeni ndugu zangu MSCL msisubiri fedha za bajeti ya Serikali. Ombeni dhamana ya Serikalimkope mnunue meli mpya mjiendeshe kibiashara. Fedha za namna hiyo zipo nyingi duniani," Alishauri.

Mradi huo umegharinu Shilingi Bilioni 8.4 na unatekelezwa na kampuni ya KTMI Co. Ltd ya nchini Korea.

Baada ya kukagua mradi huo alipata fursa ya kutembelea moja ya meli Konngwe Duniani ya MV Liemba ambayo Serikali imetenga Shilingi Bilioni 8.1 kwaajili ya ukarabati wa meli hiyo iliyoanza kufanya kazi mwaka 1913.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana akimsikiliza Mbunge wa Ilemela Dkt Angelina Mabula ambaye pia ni Waziri wa Ardhi mara baada ya kukagua ujenzi wa Meli ya MV Mwanza Septemba 5,2022, jijini Mwanza, akiwa katika ziara ya kukagua uhai wa Chama na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) Dkt. Ally Possi (wa nne toka kulia) akitoa maelekezo kwa Kaimu mhandisi mkuu wa MSCL Mhandisi Abel Gwanan-fyo mara baada ya ziara yake ya kukagua ukarabati wa meli ya MV Umoja mapema mwezi April, 2022. (Picha na Mwandi-shi Wizarani)

HABARI PICHA



Timu ya Michezo ya MSCL wakiwakilisha Kampuni katika michezo ya Bandari (Interport) iliyofan-yika katika viwanja vya Jamhuri Mkoani Morogoro mwishoni mwa Mwezi Septem-ba, 2022.



Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) wakiongozwa na (kutoka kushoto) Afisa Masoko Mkuu Bi. Eugenia Punjila pamoja na Afisa Habri Ndg. Edmond Rutajama, Afisa Masoko Msaidizi Ndg. Prosper Rwelengera na Baharia Kingwana Omary wakiwa katika banda la Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Maarufu Sabasaba yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Mgeni Rasmi wa Kilele cha Maonesho na Sherehe za Wakulima maarufu Nanenane kwa Kanda ya Ziwa Magharibi Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Martina Shigella akiwa pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima wakisikiliza kwa makini maelezo yanayotolewa na Afisa Masoko Mkuu wa MSCL Bi. Eugenia Punjila katika banda la MSCL kwenye maonesho hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Nyamhongolo, Jijini Mwanza.

Kamati ya USimamizi wa Miradi ya Meli za MSCL pamoja na Menejimenti ya MSCL na watumishi wa MSCL wakiwa katika eneo la Mradi wa Ukarabati wa Meli ya MV. Umoja wakipokea taarifa maendeleo ya mradi huo kutoka kwa Mkandarasi wa meli hiyo mapema mwezi Agosti,2022

MKURUGENZI MTENDAJI MSCL AELEZA MIPANGO YA SERIKALI KUBORESHA USAFIRISHAJI MIZIGO NCHI JIRANI



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Ndg. Eric Hamissi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) nchini Ndg. Eric Hamissi ameelezea mipango ya Serikali katika kuboresha usafiri na usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Dar es salaam kwenda katika nchi zisizokuwa na milango ya bahari ikiwemo Uganda, Malawi na DR Congo.

Ndg. Eric amesema kuwa ndani ya miaka mitatu ijayo MSCL inatarajia kuwa na meli tatu za kubeba mizigo jambo ambalo litaongeza uwezo wa kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam kupitia reli na hatimaye kuvushwa na meli za Kampuni hiyo bandari ya Mwanza kwenda Uganda, bandari ya Kigoma kwenda Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo na Bandari ya Kyela kwenda nchini Malawi.

Katika kusisitiza hilo amesema kuwa ukarabati wa meli ya MV Umoja utakapokamilika pamoja na ujenzi wa meli mbili mpya za mizigo katika Ziwa Victoria pamoja na Ziwa Tanganyika utaboresha mapato ya Kampuni hiyo na kufafanua kuwa mzigo unaopita bandari ya Dar es Salaam kwa sasa ni tani milioni 3 ambapo mzigo mwingi unasafirishwa kwa njia ya barabara kwenda katika nchi za Jirani jambo ambalo linachelewesha mizigo hiyo kufika katika nchi hizo.

"Mizigo hiyo kwa sasa inapita kwa njia ya barabara kwenda nchi za DR Congo pamoja na Uganda na hivyo hatuwezi kushindana na mtu mwenye reli, sasa sisi kabla hata ya reli ya SGR, hii reli tuliyonayo tukiijumuisha na water transport (usafiri wa njia ya maji) kwa kutumia wagon ferry (meli za kubeba mizigo) zetu tutapunguza gharama za usafirishaji kwa asilimia si chini ya 40, hivi nani atatumia barabara tena?" Alihoji

Aidha aliwatoa hofu wanaoiogopa bandari ya Mombasa inayopitisha asilimia 98 ya mizigo inayokwenda nchini Uganda ukilinganisha na asilimia 2 inayopita bandari ya Dar es salaam na kuongeza ushirikiano wa MSCL na TPA utatanua wigo wa kusafirisha bidhaa zinazokwenda Uganda kutoka bandari ya Dar es salaam kutoka asilimia 2 zilizopo hadi kufikia asilimia 20.

Ndg. Eric ameyasema hayo jana tarehe 29.08.2022 wakati akifungua kikao cha Kamati Tendaji cha Baraza Kuu la Wafanyakazi wa MSCL ambapo pia alitumia fursa hiyo Kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL.

Akitoa neno la Shukrani kabla ya kuendelea kwa kikao hicho Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Shughuli za Meli na Bandari Tanzania (DOWUTA) Ndg. Edesius Kinunda alimpongeza ndg Eric Hamissi kwa kurejea MSCL na kueleza kuwa alipoteuliwa kwenda TPA, watumishi wengi wa MSCL walihuzunika sana.

"Sina shaka na wewe kwa utendaji lakini nikuhakikishie umeacha kilio kikubwa sana kwa TPA, TPA tangu ilipoanzishwa ikianzia na THA ilipewa maneno mbalimbali kiuzalishaji, lakini utasikia bilioni 400 sijui bilioni ngapi lakini kuja kwako TPA imepata mapato ya Trilioni moja na pointi zake ni historia ambayo haijawahi kuwekwa na DG yoyote aliyewahi kupita TPA," Alisema.

NAULI MPYA

NEW VICTORIA

Hapa Kazi Tuu

MWANZA - BUKOBA
BUKOBA - MWANZA

	DARAJA	UCHUMI	BIASHARA	KWANZA
Bei ya Zamani	Mkubwa	16,000/=	30,000/=	45,000/=
	Mtoto	8,500/=	15,550/=	23,050/=
Bei Mpya (Tshs)	Mkubwa	21,000/=	40,000/=	55,000/=
	Mtoto	11,000/=	21,000/=	28,000/=

Kinana Baada Ya Kutembelea Miradi Ya Mv Mwanza Na Mt Sangara



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Kanali mstaafu Ndg. Abdulrahman Kinana (Kushoto) akiteta na Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL Eric Hamissi mara baada ya kutembelea mradi wa meli ya MV Mwanza

MWENYEKITI WA BODI ATAKA UFANISI BAADA YA KUPOKEA MELI

Inatoka Ukurasa wa kwanza

...Ameyasema hayo leo tarehe 07.09.2022 baada ya kutembelea meli tatu zilizokabidhiwa kwa MSCL pamoja na kuongea na watumishi wa Kampuni hiyo waliopo tawi la Kyela, Mkoani Mbeya katika bandari ya Itungi na Kiwira, Ziwa Nyasa.

Awali akitoa taarifa ya tawi hilo Kaimu Meneja Tawi wa MSCL Zacharia Mbilinyi alisema kuwa hivi sasa Kampuni hiyo inamiliki meli tano katika Ziwa Nyasa na idadi hiyo imeongezeka baada ya kukabidhiwa meli tatu kutoka TPA pamoja na meli mbili zilizokuwepo kabla ya kusimama kutoa huduma mwaka 2017.

"Meli hizi zinatoa huduma katika bandari 15 zilizoko katika mwambao wa Ziwa Nyasa katika Mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma ambapo kwa Mkoa wa Mbeya meli hizi zinatoa huduma katika bandari ya Itungi, Kiwira na Matema," Alisema.

Meli za MSCL zilizokuwa zikitoa huduma katika Ziwa Nyasa ni MV. Songea yenye uwezo wa kubeba abiria 212 na tani 45.5 za mizigo pamoja na MV Iringa yenye uwezo wa kubeba abiria 139 na tani 5 za mizigo ambazo zilijengwa mwaka 1974.

MARINE SERVICES COMPANY LTD
KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

Tutembelee kwenye mitandao yetu ya kijamii
Kampuni ya Huduma za Meli
mscltz MSCLtz Meli TV

Mv Liemba yatengewa shilingi Bilioni 8.1 kwa ajili ya ukarabati

Na Abdulrahman Salim

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)Meja Jenerali Mst. John Mbungo amempongeza Rais wa awamu ya sita Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga Shilingi Bilioni 45.1 kwa ajili ya kujenga meli mpya pamoja na kuzikarabati meli zilizokuwa hazitoi huduma kwa wananchi katika ziwa Tanganyika.

Pongezi hizo amezitoa tarehe 17.08.2022 baada ya kukagua mradi wa ukarabati wa meli ya kubeba mafuta ya MT Sangara pamoja na kuzitembelea meli ya MV Mwongozo na meli kongwe ya MV Liemba zilizopo katika bandari ya Kigoma, mkoani Kigoma.

"Kwakweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutoa fedha nyingi sana katika miradi hii na kuhakikisha kwamba meli zetu zinakarabatiwa, mbeli ambazo zinahitaji kutoa huduma ndani ya maji haya ya maziwa makuu, zifanye kazi na kuwafikia majirani

"Kwakweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutoa fedha nyingi sana katika miradi hii na kuhakikisha kwamba meli zetu zinakarabatiwa, mbeli ambazo zinahitaji kutoa huduma ndani ya maji haya ya maziwa makuu, zifanye kazi na kuwafikia majirani," Alisema.

Awali akitoa taarifa kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, ndg Philemon Bagambilana alisema kuwa, mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ya Awamu ya Sita imetenga shilingi bilioni 113 kwaajili ya utekelezaji wa ujenzi wa meli huku Shilingi Bilioni 45.1 zitatekeleza miradi mitano katika Ziwa Tanganyika.

"Katika fedha hizo miradi mitano itatekelezwa Ziwa Tanganyika ikiwemo ujenzi wa chelezo cha kujengea meli maana kilichopo ni kikongwe na ndio kilichotumika kujengea MV Liemba ambacho kina zaidi ya miaka 100, sasa hizi meli kubwa zinazokuja kujengwa, hii miundombinu haiwezi 'ku-support' (kuhimili), kwahiyo serikali katika mwaka huu wa fedha itajenga chelezo kipya,"Alielezea.

Akitoa mchanganuo wa fedha hizo Meneja Tawi la MSCL Mkoani Kigoma ndg. Allen Butembero alisema kuwa meliya MV Liemba imetengewa shilingi bilioni 8.1, Ujenzi wa meli mpya ya mizigo itakayokuwa na uwezo wa kubeba tani 3,000 imetengewa shilingi bilioni 12, na Ujenzi wa meli mpya ya itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo imetengewa shilingi bilioni 12.

"Tunatarajia miradi hii ikikamilika itaweza kufufua tawi hili la Kigoma pamoja na kuleta tija kwa wananchi waishio katika mwambao wa Ziwa Tanganyika kwani itapunguza gharama za usafirishaji wa abiria na mizigo."



Meli ya MV Liemba katika Ziwa Tanganyika, Mkoani Kigoma.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi MSCL Meja. Jenerali. Mst. John Mbungo akiwa katika picha ya pamoja na menejimenti ya MSC na watumishi wa MSCL tawi la Kigoma.

SHUKRANI ZA KIPEKEE KWA KUFANIKISHA JARIDA HILI

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI - PHILEMON BAGAMBILANA
MHARIRI - ABDULRAHMAN SALIM

WAJUMBE

ANSELM NAMALA
BARAKA BIGAMBO
MHANDISI ABEL GWANAFYO
NAHODHA BEMBELE NG'WITA

MARINE SERVICES COMPANY LTD
KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

HALIUZWI

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

MSCL yatoa sababu za kupanda kwa nauli

Na Abdulrahman Salim

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Ndg. Philemon Bagamilana ameutaarifu umma kuwa miongoni mwa sababu zilizopelekea kupanda kwa nauli abiria katika meli zinazotoa huduma katika Ziwa Victoria kuwa ni pamoja na kupanda kwa gharama za uendeshaji wa meli.

Ndg. Bagambilana ameyasema hayo tarehe 06.07.2022 katika mkutano na vyombo vya Habari wakati akitoa ufafanuzi wa sababu zilizopelekea kupanda kwa nauli za abiria katika meli za meli za New Butiama Hapa Kazi Tu pamoja na Meli ya New Victoria Hapa Kazi.


Aidha aliongeza kuwa uendeshaji wa meli hizo unajumuisha utunzaji wa meli baada ya kipindi cha matazamio kuisha tangu kukamilika kwa ukarabati mkubwa uliofanyika katika meli hizo mwaka 2020 na kukabuidhiwa rasmi mwaka 2021.

"Ikumbukwe kuwa mara ya mwisho bei hii ya daraja la uchumi ilibadilika mwezi Novemba,2011 na bei za daraja la Kwanza na daraja la Biashara ilibadilika mwezi Agosti, 2020," Alisema.

"Kuanzia tarehe 4.7.2022 Bei ya Daraja la Kwanza kwa Meli ya New Victoria Hapa Kazi tu ni Shilingi 55,000 huku mtoto ni Shilingi 28,000. Daraja la Biashara ni Shilingi 40,000 na mtoto ni shilingi 21,000 na Daraja la Uchumi ni Shilingi 21,000 na mtoto ni Shilingi 11,000."

"Kwa meli ya Meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu bei ya Daraja la Biashara ni Shilingi 12,000 na mtoto ni Shilingi 7,000 na Daraja la Uchumi ni Shilingi 10,000 na Mtoto ni Shilingi 6,000," Alifafanua.

Vile vile alitoa tafsiri ya anaelipa nauli yam toto kuwa ni wale wenye umri kuanzia miaka 5 hadi 11, na wenye umri wa chini ya miaka mitano hawalipii na kubainisha kuwa mabadiliko hayo ya nauli pia ni utekelezaji wa Tangazo la Serikali namba 457 la tarehe 24.06.2022 lililotolewa na Shirika la Uwakala wa Meli nchini yaani TASAC ambalo lilitoa ukomo wa ongezeko la bei hizo.



Baadhi ya Abiria wakiwa wameshuka kutoka katika meli ya New Victoria hapa kazi tu wakitokea Bukoba, Mkoani Kagera.

KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI (MSCL)
BANDARI YA MWANZA KASKAZINI, JENGO LA TPA, SAKAFU YA PILI
S. L. P. 2385, MWANZA, Hotline: +255 739 606 600
Barua Pepe: info@mscl.co.tz Tovuti: www.mscl.co.tz
Kampuni ya Huduma za Meli MSCLtz msclltz Meli TV